


Na David Azaria

MWISHONI mwa wiki iliyopita kundi kubwa la wananchi wa Mji wa Geita waliandamana hadi katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Geita, Manzie Mangochie, wakipinga kitendo cha kuuawa kwa mwanafunzi mmoja wa Shule ya Msingi Kivukoni Mjini Geita, kwa tuhuma za kukamatwa akiiba vyuma chakavu ndani ya Mgodi wa Geita.

Pamoja na kupinga mauaji hayo, walikataa kuuzika mwili wa marehemu ikiwa ni pamoja na kuutoa katika chumba cha kuhifadhia maiti cha hospitali ya wilaya, wakitaka uongozi wa mgodi huo kushughulikia zoezi zima la mazishi ya mwanafunzi huyo Hoja Juma.

Katika viwanja vya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, wananchi hao walidai wamechoshwa na vitendo vya mauaji ya raia, ambavyo vimekuwa vikifanywa na walinzi wa Mgodi wa Dhabu wa Geita (GGM) dhidi ya wananchi wanaoingia ndani ya mgodi huo kuiba vyuma chakavu na miamba taka inayotupwa kama uchafu.

Mwanafunzi huyo alipigwa risasi na walinzi wa mgodi huo kwenye ubavu wake wa kulia. Kwa mujibu wa taarifa ya uchunguzi wa daktari aliyeufanyia uchunguzi mwili wa marehemu, kifo cha marehemu kilisababishwa na kuvuja damu nyingi iliyosababishwa na kuharibiwa vibaya kwa mapafu yake na risasi.

Wakizungumza na Kaimu Mkuu wa Wilaya hiyo Moses Minga ambaye ni Katibu Tawala wa wilaya hiyo, wanasema kumekuwepo na mauaji ya mara kwa mara ndani ya mgodi huo ambayo yamekuwa yakifanywa na walinzi wa mgodi huo. Wanatoa mfano kwamba katika eneo linalozunguka kiwanja cha Ndege cha Mgodi huo, kumejaa harufu mbaya inayotokana na mizoga wananchi wanaouawa na walinzi hao.

"Kuna ushahidi wa kutosha kwamba mauaji dhidi ya raia, yamekithiri ndani ya mgodi wa Geita, mauaji yanayofanywa na walinzi wa Mgodi. Ukipita kwenye eneo la uwanja wa Ndege wa Mgodi kumejaa harufu ya mizoga, sisi tunaingia huko mara kwa mara. Lakini cha ajabu ni kwamba Serikali imekaa kimya, haijali maisha ya wananchi wake, na hata wanaoingia humo mgodini hawapendi lakini wanavumilia kwa sababu ya maisha magumu," anasema mwandamanaji mmoja mbele ya katibu Tawala, aliyejitambulisha kwa jina la Valence Wilson.

"Wanaoingia wote humo ndani ni kwa sababu ya shida zinazowakabili pamoja na kukosa maeneo ya uchimbaji, ndio maana wanaingia humo kuchukua magwangala kwa ajili ya kupata dhahabu ili waweze kumudu maisha yao, lakini kibaya zaidi wanakutana na vifo huko Serikali ikiwa imekaa kimya bila kukemea ama kutafuta muafaka kwa pande zote mbili" anaongeza.

Mara kadhaa nimeandika makala katika gazeti hili, nikielezea kero kubwa wanaywananchi ... labda nachochea vurugu. Hapana! Najaribu kutoa tahadhari, kwa sababu kuna msemo wa Kiswahili usemao kuwa "Usipoziba ufa utajenga ukuta".

Suala la 'magwangala' limekuwa ni tatizo kubwa na kila kukicha, linazidi kuchukua kasi kubwa wilayani hapa. Hali hiyo inazidisha chuki kati ya wananchi wa kawaida na wachimbaji wadogo, kwa sababu wachimbaji wengi wadogo ni wakazi wa wilaya hiyo ambao pia wana ndugu wanaowategemea, kwa ajili ya kuendesha maisha yao ya kila siku.

Hakuna ubishi kwamba kwa sasa kwamba suala la magwangala, limezidisha uwepo wa mawasiliano mabovu kati ya wananchi wa wilaya hiyo pamoja na mgodi wa Geita. Kwa kifupi naweza kusema kwamba kama suala hilo, kama halitatafutiwa ufumbuzi wa haraka, ipo siku litasababisha maafa makubwa.

Moja ya matokeo mabaya ya maandamano hayo ni kuwa hivi karibuni wachimbaji pamoja na wananchi wa mji wa Geita, walifanya vurugu kubwa na kuharibu mali mbalimbali za raia, ikiwa ni pamoja na kuchoma moto magari ya mgodi na kupasua vioo vya magari ya raia wa kawaida.

Suala la mahusiano mabaya kati ya wananchi wa wilaya hiyo na uongozi wa mgodi, lipo tangu kuanzishwa ... yanaripotiwa kwamba ikitokea bahati mbaya mtu akateleza, ni wazi kwamba uhai wake unaishia hapo hapo, kwa kuwa wanapenya na kupita katikati ya miamba iliyochongoka, kutokana na uchimbaji uliofanywa kitaalamu, huku chini ya miamba hiyo kukiwa na maji yenye kina kirefu.

Kuna taarifa kuwa baadhi ya wachimbaji hao, wamepoteza maisha kutokana na kutumbukia ndani ya mashimo hayo. Wengine wamefukiwa ndani ya mashimo ya dhahabu na wenzao wakati wa kuiba mawe hayo ya dhahabu. Wengine wametumbukia ndani ya maji na kupoteza maisha.

Kibaya zaidi, kwa sasa imefikia hatua ambapo risasi za moto zinaanza kutumika dhidi ya raia kutoka kwa walinzi wa mgodi huo na kusababisha vifo. Hali hii ni ya hatari na inapaswa hatua za haraka zichukuliwe. Vinginevyo, ipo siku hali ya hewa itachafuka ambapo watu watatafuta milango ya kupitia, lakini haitaonekana.

Kuna haja kwa viongozi wa Serikali katika Mkoa wa Geita, wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Magalula Said Magalula, wakaketi chini na kuangalia namna ya kutafutia ufumbuzi wa kudumu wa suala hili la vurugu na maandamano ya mara kwa mara.



Na David Azaria

MWISHONI mwa wiki iliyopita kundi kubwa la wananchi wa Mji wa Geita waliandamana hadi katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Geita, Manzie Mangochie, wakipinga kitendo cha kuuawa kwa mwanafunzi mmoja wa Shule ya Msingi Kivukoni Mjini Geita, kwa tuhuma za kukamatwa akiiba vyuma chakavu ndani ya Mgodi wa Geita.

Pamoja na kupinga mauaji hayo, walikataa kuuzika mwili wa marehemu ikiwa ni pamoja na kuutoa katika chumba cha kuhifadhia maiti cha hospitali ya wilaya, wakitaka uongozi wa mgodi huo kushughulikia zoezi zima la mazishi ya mwanafunzi huyo Hoja Juma.

Katika viwanja vya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, wananchi hao walidai wamechoshwa na vitendo vya mauaji ya raia, ambavyo vimekuwa vikifanywa na walinzi wa Mgodi wa Dhabu wa Geita (GGM) dhidi ya wananchi wanaoingia ndani ya mgodi huo kuiba vyuma chakavu na miamba taka inayotupwa kama uchafu.

Mwanafunzi huyo alipigwa risasi na walinzi wa mgodi huo kwenye ubavu wake wa kulia. Kwa mujibu wa taarifa ya uchunguzi wa daktari aliyeufanyia uchunguzi mwili wa marehemu, kifo cha marehemu kilisababishwa na kuvuja damu nyingi iliyosababishwa na kuharibiwa vibaya kwa mapafu yake na risasi.

Wakizungumza na Kaimu Mkuu wa Wilaya hiyo Moses Minga ambaye ni Katibu Tawala wa wilaya hiyo, wanasema kumekuwepo na mauaji ya mara kwa mara ndani ya mgodi huo ambayo yamekuwa yakifanywa na walinzi wa mgodi huo. Wanatoa mfano kwamba katika eneo linalozunguka kiwanja cha Ndege cha Mgodi huo, kumejaa harufu mbaya inayotokana na mizoga wananchi wanaouawa na walinzi hao.

"Kuna ushahidi wa kutosha kwamba mauaji dhidi ya raia, yamekithiri ndani ya mgodi wa Geita, mauaji yanayofanywa na walinzi wa Mgodi. Ukipita kwenye eneo la uwanja wa Ndege wa Mgodi kumejaa harufu ya mizoga, sisi tunaingia huko mara kwa mara. Lakini cha ajabu ni kwamba Serikali imekaa kimya, haijali maisha ya wananchi wake, na hata wanaoingia humo mgodini hawapendi lakini wanavumilia kwa sababu ya maisha magumu," anasema mwandamanaji mmoja mbele ya katibu Tawala, aliyejitambulisha kwa jina la Valence Wilson.

"Wanaoingia wote humo ndani ni kwa sababu ya shida zinazowakabili pamoja na kukosa maeneo ya uchimbaji, ndio maana wanaingia humo kuchukua magwangala kwa ajili ya kupata dhahabu ili waweze kumudu maisha yao, lakini kibaya zaidi wanakutana na vifo huko Serikali ikiwa imekaa kimya bila kukemea ama kutafuta muafaka kwa pande zote mbili" anaongeza.

Mara kadhaa nimeandika makala katika gazeti hili, nikielezea kero kubwa wanay-

labda nachochea vurugu. Hapana! Najaribu kutoa tahadhari, kwa sababu kuna msemo wa Kiswahili usemao kuwa "Usipoziba ufa utajenga ukuta".

Suala la 'magwangala' limekuwa ni tatizo kubwa na kila kukicha, linazidi kuchukua kasi kubwa wilayani hapa. Hali hiyo inazidisha chuki kati ya wananchi wa kawaida na wachimbaji wadogo, kwa sababu wachimbaji wengi wadogo ni wakazi wa wilaya hiyo ambao pia wana ndugu wanaowategemea, kwa ajili ya kuendesha maisha yao ya kila siku.

Hakuna ubishi kwamba kwa sasa kwamba suala la magwangala, limezidisha uwepo wa mawasiliano mabovu kati ya wananchi wa wilaya hiyo pamoja na mgodi wa Geita. Kwa kifupi naweza kusema kwamba kama suala hilo, kama halitatafutiwa ufumbuzi wa haraka, ipo siku litasababisha maafa makubwa.

Moja ya matokeo mabaya ya maandamano hayo ni kuwa hivi karibuni wachimbaji pamoja na wananchi wa mji wa Geita, walifanya vurugu kubwa na kuharibu mali mbalimbali za raia, ikiwa ni pamoja na kuchoma moto magari ya mgodi na kupasua vioo vya magari ya raia wa kawaida.

Suala la mahusiano mabaya kati ya wananchi wa wilaya hiyo na uongozi wa mgodi, lipo tangu kuanzishwa

yanaripotiwa kwamba ikitokea bahati mbaya mtu akateleza, ni wazi kwamba uhai wake unaishia hapo hapo, kwa kuwa wanapenya na kupita katikati ya miamba iliyochongoka, kutokana na uchimbaji uliofanywa kitaalamu, huku chini ya miamba hiyo kukiwa na maji yenye kina kirefu.

Kuna taarifa kuwa baadhi ya wachimbaji hao, wamepoteza maisha kutokana na kutumbukia ndani ya mashimo hayo. Wengine wamefukiwa ndani ya mashimo ya dhahabu na wenzao wakati wa kuiba mawe hayo ya dhahabu. Wengine wametumbukia ndani ya maji na kupoteza maisha.

Kibaya zaidi, kwa sasa imefikia hatua ambapo risasi za moto zinaanza kutumika dhidi ya raia kutoka kwa walinzi wa mgodi huo na kusababisha vifo. Hali hii ni ya hatari na inapaswa hatua za haraka zichukuliwe. Vinginevyo, ipo siku hali ya hewa itachafuka ambapo watu watatafuta milango ya kupitia, lakini haitaonekana.

Kuna haja kwa viongozi wa Serikali katika Mkoa wa Geita, wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Magalula Said Magalula, wakaketi chini na kuangalia namna ya kutafutia ufumbuzi wa kudumu wa suala hili la vurugu na maandamano ya mara kwa mara.



Wananchi wa Mji wa Geita wakifanya maandamano kupinga kuuawa kwa mwanafunzi wa darasa la sita, Hoja Juma wa Shule ya Msingi Kivukoni. Tukio hilo linadaiwa kufanywa na walinzi wa Mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGM).

# Vurugu Geita zaendelea kuwatesa viongozi wake




Mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGM).

oipata wachimbaji wadogo wa Wilaya ya Geita, ambapo maeneo yapo mengi yamechukuliwa na wawekezaji wakubwa, kwa ajili ya shughuli za uchimbaji na utafiti wa madini. Lakini, kibaya zaidi hata watafiti wenyewe, wamekuwa wakihodhi maeneo hayo kwa muda mrefu bila kuyaachia.

Hakuna ubishi kwamba hatua waliyofikia wananchi wa Wilaya ya Geita sasa ni kubwa. Kama serikali za wilaya na mkoa hazitakuwa makini katika kutatua mgogoro huo, unaofuka moshi kwa sasa, kuna siku ambayo kutakuja kuibuka vurugu kubwa, ambazo zitasababisha maafa yasiyoelezeka.

Nasema hivyo kwa sababu hizi vurugu na maandamano tunayoyaona, hayajaanza leo Geita bali yanafanyika mara kwa mara. Hili ni funzo tosha kwa vyombo vya Serikali pamoja na viongozi wa Serikali, kwamba kuna dalili mbaya zinakuja.

Sitaki kueleweka kwamba labda nachochea vurugu. Ha...

mgodi huo miaka 10 iliyopita. Lakini, kwa sasa naweza kuthibitisha kwamba 'Magwangala' yamezidisha mahusiano hayo kuwa mabovu zaidi ya mara 100!

Nasema hivyo kwa sababu katika kipindi chote hicho cha mahusiano mabovu, kati ya wananchi na mgodi huo, sio kwamba wananchi walikuwa hawalalamiki. Walikuwa wanalalamika chini kwa chini, ingawa kwa sasa chuki imekuwa ya hadharani na sio kificho tena.

Kibaya zaidi ni kwamba wanaolalamika na kufanya vurugu ni vijana, ambao ndio wanaaminika kujihusisha zaidi na shughuli za uchimbaji wa madini. Lakini, inaelezwa kwamba vijana ndio wenye uwezo wa kuvuka milima na mabonde kabla ya kuingia na kutoka ndani ya mgodi huo, huku ikielezwa kwamba maeneo wanayokwenda kuiba mawe ya dhahabu ni ya hatari kubwa.

Kuna maeneo mengine ndani ya Mgodi huo wa Geita, yanaripotiwa kwamba iki...